Research Article

Section: Literature, Linguistics & Criticism

Check for updates

Published in Nairobi, Kenya by Royallite Global.

Volume 5, Issue 1, 2024

**Article Information**
Submitted: 18th February 2024
Accepted: 25th March 2024
Published:13th April 2024

Additional information is available at the end of the article

https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/

To read the paper online, please scan this QR code

**How to Cite:**
Uchanganuzi wa mahusiano ya kitabaka katika riwaya za Kuli na Pendo la Karaha. (2024). *Research Journal in African Languages, 5*(1). https://royalliteglobal.com/african-languages/article/view/1550

# Analyzing social class relations in Shafi's *Kuli (1979)* and *Habwe's Pendo la Karaha (2014)*

**Virginia Wambui Mwathi, Vifu Makoti and John Mutua**
Department of Linguistics and Languages, Machakos University, Kenya
Correspondence: virginiamwathi6@gmail.com
https://orcid.org/0000-0002-5054-1740

**Abstract**
The society we are in, is of an economic construct that enables a few individuals to own and control means of production. Courtesy to this characteristic, social classes emerge; the upper class, made up of the haves and the lower class made up of the have nots. These social classes are always interracting, bounded by the process of production and gain livelihood. This necessitates an interdependence. From this interaction, this article will investigate the nature of the relationships of the social classes. These relationships will be analyzed in their positive and negative aspects. The study will be guided by the Marxist theory. The theory rules supreme in all discussions partaining to social classes.

**Keywords:** Social class, relationships, exploitation, Marxism

© 2024 The Author(s). This open access article is distributed under a Creative Commons Attribution (CC-BY-NC-SA) license.

Research Article

Section: Literature, Linguistics & Criticism

Published in Nairobi, Kenya by Royallite Global.

Volume 5, Issue 1, 2024

**Article Information**
Submitted: 18th February 2024
Accepted: 25th March 2024
Published:13th April 2024

Additional information is available at the end of the article

https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/

To read the paper online, please scan this QR code

**How to Cite:**
Uchanganuzi wa mahusiano ya kitabaka katika riwaya za Kuli na Pendo la Karaha. (2024). *Research Journal in African Languages, 5*(1). https://royalliteglobal.com/african-languages/article/view/1550

# Uchanganuzi wa mahusiano ya kitabaka katika riwaya za *Kuli* na *Pendo la Karaha*

**Virginia Wambui Mwathi, Vifu Makoti and John Mutua**
Department of Linguistics and Languages, Machakos University, Kenya
Correspondence: virginiamwathi6@gmail.com
https://orcid.org/0000-0002-5054-1740

**Ikisiri**
Jamii tuliyomo, ni yenye mfumo wa kiuchumi unaoruhusu watu wachache kumiliki na kudhibiti njia kuu za uzalishaji mali. Kutokana na sifa hii, matabaka hujitokeza: tabaka la juu ambalo ni la walionavyo, na tabaka la chini ambalo ni la wasionavyo. Matabaka haya hayakosi kutangamana katika mchakato wa uzalishaji mali na vilevile utafutaji wa riziki.Yote mawili hutegemeana. Kutokana na kutangamana kwao, makala hii itachunguza mahusiano ya matabaka haya ni ya aina gani. Mahusiano haya yatachunguzwa kwa kuangalia uhasi ama uchanya wake. Nadharia ya Umarx itaongoza utafiti huu. Ni nadharia inayotawala mijadala yote inayohusu utabaka.

**Istilahi muhimu:** Tabaka, Mahusiano, unyonyaji, Umarx

© 2024 The Author(s). This open access article is distributed under a Creative Commons Attribution (CC-BY-NC-SA) license.

**Utangulizi**

Kwa kawaida matabaka hayakosi kutagusana kutokana na haja yao ya kutegemeana. Tabaka la juu, hutegemea la chini kulifanyia kazi huku la chini likitegemea la juu ili lipate riziki baada ya kufanyia lile la juu kazi. Marx katika *Communist Manifesto*, anadai kuwa mfanyakazi hupata ajira kutoka kwa bepari ikiwa tu nguvukazi yake inasababisha kuongezeka kwa mtaji. Hii ni sawa na kusema kuwa, atapata ajira ikiwa tu nguvukazi yake inampa bepari faida (Ball na Dagger, 2005). Kwa hivyo, kutagusana huku kunafaidi pande zote mbili. Kutokana na mtagusano kati ya tabaka la juu na la chini, uhusiano wao unaweza ukawa chanya ama hasi. Wapo waajiri ambao hawacheleweshi malipo ya wafanyakazi wao, huwapa malazi mazuri na lishe bora. Pia, waajiri hawa huwalipia hata kozi wapate ufahamu wa stadi fulani, huwasamehe wanapokosea ama kuwaadhibu kwa njia ya utu na hata kugharamika wanapoumia ama kuugua wakiwa kazini. Vilevile, wapo viongozi wanaowajibika katika uongozi kwa kutimiza ahadi zao kwa wananchi. Hii ni mifano ya uhusiano chanya kati ya tabaka la juu na la chini. Tukio la wafanyakazi kususia kazi kutokana na hali duni za kazi kama vile: kupigwa, kunyimwa ruhusa ya mapumziko, kukosa kulipwa, kudhulumiwa kimapenzi na viongozi wasiowajibika katika uongozi, ni mifano ya uhusiano hasi kati ya matabaka haya. Katika makala hii, uchanya na uhasi wa mahusiano haya unabainishwa kwa kujikita katika uhusika. Marx anadai kuwa, historia ya mwanadamu ndiyo historia ya utabaka. Kwa hivyo, tutaonyesha harakati za kitabaka zinazodhihirika katika riwaya teule.

**Mahusiano ya Kitabaka katika Riwaya za *Kuli* na *Pendo la Karaha***

Riwaya hizi zimedhihirisha uhusiano uliopo baina ya matabaka kutokana na mtagusano wa wanajamii wa tabaka la juu na la chini. Katika riwaya hizi, kuna mwajiri na mwajiriwa, mtawala na mtawaliwa na maskini na matajiri.

**Mwajiri kama Mnyonyaji**

Mnyonyaji ni mtu anayetumia watu ama vitu kwa manufaa yake mwenyewe bila kujali maslahi ya anaowatumia. Mfano wa tukio la unyonyaji ni pale ambapo mfanyakazi hufanya kazi kwa saa za ziada ama kazi nyingi na ngumu kwa malipo duni sana yasiyolingana na nguvukazi yake. Matukio ya unyonyaji yamekuwepo katika jamii tunayoishi. Shirika la Kimataifa la Wafanyakazi (ILO) liligundua matukio ya unyonyaji katika mazingira ya kazi. Liligundua kuwa, wapo wafanyakazi wanaolipwa mshahara mdogo sana, mshahara usiolingana na kazi wanayoifanya (ILO, 2019). Pia ilidhihirika kuwa, kuna wafanyakazi wanaofanya kazi kwa muda wa ziada bila malipo na hali duni za kazi kama vile kukosa kulindwa kutokana na kemikali na hata mashine zinazoweza kumdhuru mfanyakazi (ILO, 2021). Matukio haya ya unyonyaji, yanaakisi ukweli wa dai la Marx katika Ball na Dagger (2005) kuwa, katika jamii ya kibepari, mfanyakazi huwa mtumwa wa tabaka la mabepari, mashine za kazi na pia wasimamizi wake kazini. Unyonyaji unadhihirika katika riwaya hizi teule.

Katika riwaya ya *Kuli,* Rashidi anamwambia Mzee Tindo ambaye ni msimamizi wao kazini kuwa yeye (Rashidi), pamoja na wafanyakazi wenzake, wanahisi kuwa kazi wanayoifanya ni kubwa na malipo wanayopata ni madogo. Wanamwomba mzee huyu wafanye utaratibu waongezewe pesa (uk.48). Tunaendelea kupata mfano ufuatao:

> Mfano 1:
> ...Ilivyokuwa hali ya maisha katika nchi iko juu basi tunadai nyongeza katika malipo. Mara nyingi tunafanyishwa kazi wakati saa za kazi zimekwisha, basi tunadai pindi ikiwa kazi kama hiyo imetokezea basi tulipwe mara mbili zaidi...tunadai tupatiwe nguo za kazi, vilevile tunadai kila mfanyakazi awe na

dhamana...

(kur.64-65)

Hii ni barua iliyoandikwa na wafanyakazi wa bandarini kwa waajiri wao ikidai kuwa wamechoka kunyonywa na kukandamizwa na kampuni hiyo. Malalamishi yao katika barua hii yanadhihirisha kuwa mwajiri wao ana tabia ya unyonyaji kwa vile anawatelekeza wafanyakazi. Tukio lingine la unyonyaji ni kama lifuatalo:

Mfano 2:
"Nataka kujua mna shauri gani kuhusu Manafi?" Faraji aliuliza
"Habari ya Manafi? Habari ya Manafi hakuna shauri!...Manafi alikuwa mtu wa *daily pay* kampuni haiwezi kumfikiria chochote," George alisema...

(uk.82)

Maneno ya George katika dondoo hili yanamchora kama mnyonyaji na mkatili kwa vile hajali yaliyompata Manafi aliyekuwa mfanyakazi wake. Hii ni baada ya Manafi kuzama baharini na kuaga dunia baada ya kuangukiwa na gunia la sukari. Tunatarajia George angefuatilia kisa kile na hata kushughulika kwa kufidia familia ya Manafi.

Tendo la kuwalipa wafanyakazi mishahara midogo baada ya kazi nyingi na hata kunyimwa malipo kwa kufanya kazi kwa muda wa ziada ni kiashiria cha unyonyaji. Mwajiri anataka kupata faida kubwa kwa kuezeka pesa chache. Aidha, mfanyakazi kunyimwa fidia baada ya ajali, dhamana na hata nguo za kazi kunaonyesha namna mwajiri asivyojali maslahi ya mfanyakazi wake. Hiki ni kiashiria cha unyonyaji kwa vile, mwajiri anamtumia mfanyakazi kwa manufaa yake mwenyewe.

Katika riwaya ya *Pendo la Karaha,* Lindo ambaye hufanya kazi ya kuuza dawa za kulevya anamweleza Kudra kuwa anataka kutoka kwenye utumwa huo. Lindo anasema,

Mfano 3:
Dadangu, nataka kutoka kwenye utumwa huu. Ninatajirisha watu. Wanaendesha *Mavolvo, Mercedes Benz, Malandrover, Discovery* na mimi mwenyewe ni mtumwa. Silali. Kisa na maana ni kuzungusha dawa angalau nimlipe mkubwa wangu.

(uk.31)

Kwa kusema hivi, Lindo anamaanisha kuwa anatamani kuacha kazi hii ya uuzaji wa dawa za kulevya lakini anashindwa kuacha. Anamwonya Kudra dhidi ya kujiunga na biashara hii. Lindo kutumika na matajiri kuuza dawa bila yeye kulala wala kutajirika, huku wakubwa wake wakitajirika, ni mfano wa unyonyaji.

Waajiri wa Kudra ( Aminii na Nayrat) wana tabia za unyonyaji pia. Wanamwambia Kudra,

Mfano 4:

" Wajua tulisahau kukata gharama ya ndege katika mshahara wako. Pole kama itakuathiri vibaya lakini lazima tufanye hivyo. Itabidi pia tukukate pesa za ajenti wako, mama Rehema...Pia, biashara yetu haiendi vizuri. Itabidi tuukate mshahara wako..."

(kur.87-88)

Kwa maoni yetu, huu ni unyonyaji kwa sababu baada ya kukatwa mshahara, kazi yake haijapunguzwa katika lile boma. Hii ina maana kuwa, mapato yake hayatalingana na kazi anayoifanya. Itakuwa ni ya sulubu na huo ni unyonyaji kwa upande wa mwajiri.

Fauziya vilevile, ni mfano wa mwajiri ambaye ana sifa ya unyonyaji. Tunaelezwa kuwa, ana biashara ya kukanda watu viungo inayoitwa '*massage parlour*'. Amewaajiri wasichana wengi pale kufanya kazi hiyo, Kudra akiwa mmoja wao. Kando na hayo, pasi zao zinawekwa na Saumu ambaye ni msimamizi. Kuwekewa pasi kunafanya iwe vigumu kutoka pale. Kwa maoni yetu, kuwekewa pasi kunawafanya kuwa watumwa wa biashara ile kwa vile ni vigumu kuondoka. Kwa hivyo, Fauziya atazidi kufaidika katika ile biashara kwa kuwanyonya wafanyakazi wake huku wafanyakazi wakiumia. Mwishowe, Kudra anakosa kufuata maagizo ya kazi na kusema kuwa haitaki. Hii ni baada ya kugundua kuwa Fauziya ameweka wasichana chungu nzima katika hilo jengo kwa malipo duni ili kujinufaisha (uk.166).

Katika riwaya teule, inatokea kuwa uhusiano baina ya mwajiri na mwajiriwa, kwa kiwango kikubwa unamfaidi mwajiri huku mwajiriwa akinyimwa stahiki yake. Kilio cha mfanyakazi anapotetea haki zake kunaonyesha kuwa, uhusiano kati yake na mwajiri wake ni hasi. Mwajiri anaonekana kuwa mbinafsi kutokana na tabia yake ya kuthamini faida kuliko maslahi ya wafanyakazi wake. Marx katika Odetola na Ademola (1987) anazungumzia tukio hili na kusema kuwa, tabaka linalonyanyaswa hufanya kazi kwa mshahara mdogo. Hutenganishwa na mazao ya kazi zao. Katika *Communist Manifesto,* Marx anadai kuwa, kwa kawaida, malipo ya nguvukazi ni yale yanayomsaidia mfanyakazi kudumu kama mfanyakazi. Ni malipo ambayo hayabaki kumsaidia kufanya lolote la ziada baada yake kutimiza mahitaji yake ya msingi. Wakomunisti wanapigania kumalizwa kwa utumwa huu (Ball na Dagger, 2005). Kutokana na haya, ni dhahiri kuwa waajiri hutumia nguvukazi ya waajiriwa kutimiza malengo yao ya kibepari na hivyo tabia hii inawachora kama wadhalimu, wabinafsi na wanyonyaji. Hivi ni viashiria vya uhusiano hasi kati ya makundi haya mawili.

Tunamuunga mkono Eagleton (2011) anayeendeleza Umarx kwa kushtumu unyonyaji wa kibepari kwa vile anauona kama mfumo wa ulafi, unyanyasaji na vilevile uangamizaji. Kwa maoni yetu, tunapendekeza mfanyakazi kupata stahiki yake baada ya kazi, asipewe wala kulazimishwa kufanya kazi inayomkosea heshima na vilevile kulindwa kutokana na hatari zozote zinazoweza kutokea kazini. Mfanyakazi akipata stahiki yake, uhusiano kati yake na mwajiri utakuwa bora na hivyo basi watapata mazao mazuri ya kazi.

**Tabaka la Juu kama Lisilowajibika**

Kwa mujibu wa *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (TUKI, 2004) wajibu ni jambo linalomlazimu mtu kulitimiza; jambo ambalo mtu hana hiari nalo katika kulifanya; ni sharti ama jukumu. Unapokosa kufanya jukumu lako, hii ina maana kuwa umekosa kuwajibika. Kutowajibika huzaa uhusiano hasi baina ya wanajamii kwa vile imani huisha miongoni mwao na chuki kuchipuka. Matukio ya kutowajibika yanaonekana katika riwaya teule.

**Kutowajibika kwa Mwajiri**

Wajibu wa mwajiri kazini ni kuhakikisha kuwa mazingira ya kazini ni salama kwake na kwa mwajiriwa, kumpa mwajiriwa stahiki yake baada ya kazi na kumpa fidia anapoumia kazini. Hii ni mifano ya wajibu wa mwajiri. Mfanyakazi naye ana wajibu wa kufanya kazi kama alivyoelekezwa na mwajiri ama msimamizi wake. Makundi haya mawili yanapokosa kufanya haya, yamekosa kuwajibikia kazi zao. Katika utafiti huu, tumepata matukio ya kutowajibika kwa waajiri. Riwaya ya *Kuli* ina mifano ifuatayo:

Mfano 5:

"Nani tapeleka yeye hospitali?" Yule Mzungu aliuliza.
"Gari la kampuni si lipo?" Wote waliopo pale walisema kwa umoja wao.
"Ninyi hapana jua kama gari ya kampuni iko kazi mingi?"
"Muhimu hiyo kazi au huyu mtu aliyeumia? Unafikiri kazi muhimu kuliko maisha ya mtu?"Akida aliuliza kwa hamaki.
"Hiyo hapana shauri yangu," alijibu yule Mzungu na kwenda zake.

(uk.6)

Haya ni mazungumzo kati ya makuli na Mzungu ambaye ni msimamizi wao wakiwa kazini kule bandarini. Hii ni baada ya mfupa wa bega la kuli mmoja kudata, kwa sababu ya uzito wa chuma walichokuwa wakibeba. Tendo la Mzungu kusema, "Hiyo hapana shauri yangu," na kuondoka, kunaonyesha namna asivyojali wafanyakazi wake. Hiki ni kiashiria cha kutowajibika na kinaonyesha uhusiano hasi uliopo baina ya mwajiri na mwajiriwa. Wafanyakazi hawa wanatarajia kuwa mwenzao angepelekwa hospitalini kwa gari la kampuni lakini hilo halifanyiki. Mwishowe, wanachanga pesa na kumsaidia wao wenyewe (uk.7).

Kwingineko pia kunatokea kutowajibika:

Mfano 6:

"Manafi ametumbukia baharini na mpaka sasa hivi hatujamwona!" Faraji alimwambia George.
"Naanguka mwenyewe au alikuwa melewa?" George aliuliza.
"Kaangukiwa na gunia la sukari!" Faraji alijibu.
"Sasa mimi nafanya nini?" George aliuliza.

(kur.81- 82)

Mfano huu unatuonyesha mazungumzo kati ya George na Faraji ambaye ni mwakilishi wa wafanyakazi wakiwa bandarini. Hii ni baada ya kuli mmoja (Manafi) kutumbukia baharini na kutopatikana. George anaposema, "Sasa mimi nafanya nini?" ni matamshi yanayoonyesha kutojali maslahi ya wafanyakazi wake. Tabia hii inadhihirisha kuwa, uhusiano baina yao ni hasi. George, kwa uwezo wake, anatarajiwa kujali wafanyakazi wake na katika tukio hili, angejaribu kadri ya uwezo wake kutatua lile tatizo.

Katika riwaya ya *Pendo La Karaha* , matukio kama haya yanadhihirika ifuatavyo:

Mfano 7:

"Mwanangu ulimpeleka Dubai sasa nasikia anafanyiwa mateso huko," Riziki aliteta.
" Mwanao alienda kwa hiari yake, dadangu. Pia akiona si kuzuri, ana miguu na macho. Anaweza kurudi. Kama umechomwa na hasira, nenda polisi. Nenda unishtaki," Rehema alimweleza Riziki...

(kur.169-170)

Haya ni mazungumzo kati ya Riziki (mama Kudra) na Rehema ambaye ni wakala wa wasichana waendao ng'ambo kufanya kazi za nyumba. Wawili hawa wamo ofisini mwa Rehema. Riziki anamlilia mwanawe ambaye anasikia kuwa anatesekea kazini mwake nchini Dubai. Matamshi ya Rehema yanatuonyesha namna asivyojali maslahi ya wasichana anaonadi. Hiki ni kiashiria cha kutowajibika na

kinadhihirisha uhusiano hasi uliopo baina ya tabaka la juu na la chini. Kwa maoni yetu Rehema kama wakala, angeshughulika kwa kupiga simu na kujua hali ya Kudra na kumweleza mamake ili wawe na mpango wa kumsaidia lakini hili halifanyiki.

> Mfano 8:
> Kuna mmoja aliyekuwa foleni aliyeitwa Jane. Alitobolewa jicho na mtoto wa mwajiri wake. Alitazamia mwajiri wake angempa ridhaa lakini baadaye alielezwa ilikuwa ajali ya kazini. "Mtoto hakupenda, ilikuwa ajali," mwajiri wake alimweleza ukweli mchungu.
>
> (uk.175)

Haya ni maelezo ya mwandishi akitueleza kuhusu Jane, aliye katika uwanja wa ndege pamoja na wasichana wengine kama vile Kudra waliookolewa kutoka kwa mateso chini ya waajiri wao na hapa uwanjani wanangoja kusafirishwa kurudi katika nchi zao. Mwajiri wa Jane ni mfano wa mwajiri asiyewajibika. Kwa kukosa kumpa Jane fidia baada ya kutobolewa jicho na mwanawe, ni onyesho la ukatili na vilevile kutowajibika. Kutomshughulikia baada ya ajali hii na kuendelea kumpiga, kumtukana na kumnyima chakula (uk.175), ni tendo la dhuluma na huu ni uhusiano hasi kati ya wawili hawa.

Kutokana na mifano hii, inatokea kuwa mwajiri ni mtu mwenye ukatili kwa sababu ya tabia yake ya kuthamini kazi kuliko wafanyakazi wake na maslahi yao. Inadhihirika kuwa, mwajiri humwona mwajiriwa kama 'chombo' cha kazi badala ya kumwona kama 'binadamu' mwenye mahitaji kama yake. Tabia hii inadhihirisha ukweli wa dai la Barry (2009) kuwa, mwajiri humvua mwajiriwa utu wake na kumfanya 'chombo' cha uzalishaji mali kutokana na namna mwajiri anavyochukulia suala la faida na hasara kwa dhati na kutojali sana kuhusu mwajiriwa wake. Waajiri kama hawa wapo katika hali halisi ya maisha. Tabia hii ni dhuluma ambayo haifai kimaadili lakini ipo na inafaa kupingwa vikali. Ni unyanyasaji wa wafanyakazi unaopingwa na ILO.

**Kutowajibika kwa Serikali**

Serikali ni chombo ambacho kwa misingi maalum kimepewa mamlaka ya kuendesha utawala wa nchi. Serikali hutawala ikiongozwa na katiba ambayo ni jumla ya kanuni ambazo huwezesha serikali itawale au chama au kampuni iendeshe shughuli zake (*Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, 2004). Kando na katiba, kuna mikataba ya kimataifa ambayo serikali fulani huwa ndani yake ambayo pia huifuata katika utawala wake. Kwa hivyo, serikali ina jukumu la kushikilia katiba yake. Inapokosa kutii, basi imekosa kuwajibika katika majukumu yake. Serikali yenye mapendeleo, isiyofanya mgao sawa wa rasilimali miongoni mwa wananchi wake, inayonyima kundi fulani haki na kupa lingine, na kujilimbikizia mali ya umma, ni mfano wa namna ambavyo serikali inakosa kuwajibika. Serikali isiyowajibika hufanya wananchi kutokuwa na imani kwake, kuwa na machungu na wakati mwingine hata kung'atuliwa uongozini kama ilivyofanyika Ufaransa katika mapinduzi yake. Matukio ya kutowajibika yamedhihirika katika riwaya teule.

Riwaya ya *Kuli* inatupa taswira ya maisha ya Zanzibar kabla ya uhuru. Utawala ulikuwa chini ya serikali ya Uingereza. Serikali hii ilikuwa moja kati ya waasisi wa Shirika la Kimataifa la Wafanyakazi Ulimwenguni (*International Labour Organization*) lililoasisiwa mnamo mwaka wa 1919. Kwa hivyo, serikali hiyo ilikuwa na jukumu la kufuata mikataba ya shirika hili na kando na hayo, kufuata Tamko la Kimataifa kuhusu Haki za Binadamu (*Universal Declaration of Human Rights* (UDHR) lililoundwa mnamo mwaka wa 1948 na unatumika hadi leo. La kusikitisha ni kuwa, katika mtangamano wa waajiri, wafanyakazi na wanasheria katika riwaya hii, linalodhihirika ni unyanyasaji wanaofanyiwa

wafanyakazi. Katika mswada huu wa haki za binadamu, mkataba nambari 20, unaeleza kuwa, kila mtu ana haki ya uhuru wa kuungana na kuandamana kwa amani. Pamoja na hayo, mkataba nambari 7 unasema kuwa, kila mtu ana haki sawa mbele ya sheria na ana haki ya kulindwa na sheria bila ubaguzi wowote. Katika riwaya hii, wafanyakazi wanapokutana katika ofisi yao kuzungumzia maslahi yao, gari la polisi linafika na kiasi cha askari kumi na wawili wanashuka wakiongozwa na ofisa wa Kiingereza, huku wamejihami kwa virungu. Wanajilazimisha ndani ya chumba kile na kuvurumisha virungu wakipiga kila aliye karibu nao (uk.85). Tukio hili, linaonyesha kuwa wafanyakazi hawa wamenyimwa haki zinazotolewa katika mkataba nambari 7 na 20. Tunaamini kuwa, askari wangewalinda katika mkutano ule na kuwaadhibu ikiwa tu mkutano huo ungesababisha rabsha.

ILO (1928), mkataba nambari 26 unahitaji serikali kuweka sheria ya mshahara wa chini zaidi *(minimum wage fixing)* ambao mfanyakazi anafaa kupokea. Mshahara huu unafaa kumpa mfanyakazi maisha yenye heshima na unafaa kuzingatia mambo kama vile gharama ya maisha. Mwandishi wa riwaya hii anatueleza kuwa, katika barua ya wafanyakazi kwa waajiri wao, moja ya malalamishi yao ni nyongeza ya mishahara. Hii ni kwa vile gharama ya maisha imeongezeka na vilevile wanadai malipo ya muda wa ziada wa kufanya kazi (kur.64-65). La kushangaza ni kuwa, wafanyakazi hawa wanaposusia kufanya kazi, George ambaye ni mkuu wao, kwa kupiga simu tu, askari wanafika pale bandarini na kuanza kuwapiga wale makuli (kur.162-163). Kwa maoni yetu, serikali imefeli katika jukumu lake la kusikiza kilio cha wafanyakazi na kujiegemeza katika upande wa waajiri. Tendo la wafanyakazi kufumaniwa katika ofisi yao wanapokutana na kupigwa na askari wanaposusia kufanya kazi, linaonyesha kuwa serikali hii imekosa kutii mkataba nambari 87 (ILO, 1948) unaohitaji serikali kuwa na wajibu wa kuheshimu haki za wafanyakazi ya kuunda vyama na kujiunga navyo. Vilevile, kuheshimu haki yao ya kuungana kuzungumzia maslahi yao na kuchagua mwakilishi wao. Fauka ya hayo, mkataba huu unaipa serikali jukumu la kuchukua hatua ya kuzuia kudhulumiwa kwa vyama hivi na kuhakikisha kuwa vyama hivi haviingiliwi na waajiri ama serikali yenyewe. Kutowajibika huku, ni dhihirisho la uhusiano hasi kati ya tabaka tawala na wafanyakazi. Serikali ingewajibika, kusingekuwa na uhasama kati ya waajiri na wafanyakazi ama vyombo vya dola na wafanyakazi.

Jamii ya *Pendo La Karaha* ni mfano wa jamii inayotawaliwa na viongozi wasiowajibika. Maneno ya Mwamba yanadhihirisha kutowajibika kwa serikali anapodai kuwa, wanaowasukuma watoto kwenye dawa ni hao matajiri wanaoziuza dawa. Ni hao viongozi wanaochaguliwa na kufanywa wabunge na *madisii* (uk.44). Maneno ya Mwamba, kando na kumchora kiongozi kama asiyewajibika, anaonekana kama kielelezo duni kwa wananchi. Kiongozi anafaa kuwa mstari wa mbele katika vita dhidi ya dawa za kulevya kwa kutoruhusu uuzaji na utumiaji wake na hata kuhakikisha kuwa wanaojihusisha katika matumizi yake wamehukumiwa. Tunakubaliana na maoni ya Njenga (2021) anapodai kuwa, wanajamii wanafaa kufahamu kuwa wanachangia katika uongozi mbaya kwa vile wao ndio huchagua viongozi hao.

Subira ni mama ya Rukia, msichana anayeuwawa na mwajiri wake akiwa Dubai. Kisa na maana ni kuwa, mwajiri anashuku kuwa Rukia amemwibia pesa zake na dhahabu ya thamani ya milioni kumi (10,000,000). Subira anaenda Nairobi kusema na Waziri wa Mambo ya Kigeni lakini anafahamishwa kuwa yu katika likizo ya mwezi mmoja. Subira anaingia ofisi moja baada ya nyingine bila kupata usaidizi wowote. Ubalozi wa Miliki za Uarabuni (*United Arab Emirates)* unakosa pia kumsaidia kwa kudai kuwa mwanawe (Rukia) hapatikani katika data yao (kur.50-51). Mfano huu ni dhihirisho la kutowajibika kwa serikali. Baada ya kifo cha Rukia, waajiri wake hawachukuliwi hatua yoyote na serikali. Serikali ina jukumu la kulinda haki ya kila mwanadamu ya kuishi (UDHR, 1948: mkataba nambari 3). Tukio la Subira kuenda ofisi baada ya nyingine na kuambulia patupu kunaonyesha namna serikali ilivyolegea katika majukumu yake ya kutumikia wananchi. Pamoja na hayo, Rukia kunyimwa

haki ya kuishi, na mwajiri wake kutochukuliwa hatua ya kisheria ni kiashiria cha kufeli kwa serikali. Kutowajibikia huku, ni ishara ya uhusiano hasi kati ya matabaka haya. Tunapendekeza njia mbadala za kumwadhibu mfanyakazi anapokosa kama vile kufutwa kazi bali si kutoa maisha yake. Vilevile, tunapendekeza Wizara ya Mambo ya Kigeni kufuatilia hali ya maisha ya wananchi wanapokuwa ng'ambo. Vilevile, serikali inafaa kuchukua hatua za kisheria kwa yeyote anayevunja sheria bila kubagua tabaka lake. Kuwajibika kutaleta uhusiano bora kati ya matabaka husika.

Kutowajibika kwa serikali kunaendelea kuonekana pale ambapo serikali inafumbia macho matendo maovu ya Rehema ya kunadi wasichana Uarabuni wanakoenda kutesekea. Mwandishi anatueleza kuwa, serikali haikujali kuwa vinywa vya watu vililalamika. Magazeti yalilalamika lakini Rehema alitembea Changamwe kwa madaha akisuta maadui wake kwa kiburi. "Mtasema kisha mtachoka," alisema kwa kiburi (uk.56). Katika biashara ya Fauziya kule Dubai, wafanyakazi wake, Kudra akiwa mmoja wao, wanalalamikia mshahara mdogo ambao hauwawezeshi kujikimu. Pasi zao zinawekwa na Saumu ambaye ni msimamizi wao ili wasitoroke na mmoja wao anayeitwa Rose anapojaribu kutoroka baada ya maudhi haya kuendelea, anashikwa na polisi na kushitakiwa kwa kesi ya wizi. Mwishowe anajitoa uhai. Kudra haelewi ni vipi mambo yale yanatokea katika mji wa Dubai na serikali isijue. Baadaye, anakuja kuelewa kuwa askari, baada ya kupewa hongo na Fauziya, hawawezi kufanya jambo lolote au kumsikiliza yeyote (uk.168).

Tunakashifu matendo ya utoaji rushwa na kukubaliana na dai la Kandoro katika Yunus (2013) kuwa, rushwa huhatarisha upatikanaji wa haki za binadamu mfano katika kisa cha Kudra na wafanyakazi wenzake. Kandoro anapinga utoaji rushwa kwa kusema kuwa ni mbaya kwa vile huathiri ustawi na mustakabali wa taifa. Matendo ya Fauziya na Rehema yanadhihirisha ukweli wa madai ya mwanasosholojia Ritzer (2008) kuwa, mwanadamu ni mtu mwenye tamaa ya mali na kila mara hutaka kuwa ndiye mtu mwenye mali kuliko wanajamii wote. Ili kuweza kutimiza tamaa yake, hutafuta njia rahisi na ya mkato ambayo itaweza kumpatia utajiri wa haraka. Ni kutokana na hali hii, ndio maana baadhi ya wanadamu hujiingiza katika vitendo viovu. Matendo haya yanadhihirika pale tunapoona ufisadi uliopo baina ya Fauziya na serikali, Rehema na serikali na hata uovu wa uuzaji wa dawa za kulevya unaofumbiwa macho na kuchangiwa na watu wakubwa serikalini.

Machungu waliyonayo wanajamii wa *Pendo La Karaha* kutokana na kutelekezwa na serikali yanadhihirisha uhusiano hasi uliopo baina ya mtawala na mtawaliwa. Katika uchanganuzi wetu, inaonekana kuwa jamii ya mnyonge kukosa haki. Viongozi wangewajibika katika uongozi, kusingekuwa na mahusiano hasi. Suala la Wakenya kutesekea ng'ambo bila ya serikali kuingilia kati ni mojawapo ya matukio yanayodhihirisha kutowajibika kwa serikali kwa kutelekeza haki za binadamu.

Tunawashauri wananchi kutokaa kimya wanaponyanyaswa na mifumo dhalimu ya serikali. Tunaunga mkono maoni ya Munyasya (2017) anayeeleza kuwa watu hutekeleza mabadiliko kwa sababu hawajaridhika na jinsi viongozi wanavyowatawala au kwa kuchukia mifumo dhalimu ambayo hudumisha maslahi ya watu wachache wenye mamlaka. Munyasya anaendelea kuonyesha namna vijana wanavyopigana dhidi ya uongozi mbaya na kuelimisha umma dhidi ya kuchagua viongozi wadhalimu na kukaa kimya wanaponyanyaswa. Tunapendekeza serikali kuhudumia kila mwananchi kwa njia sawa bila ubaguzi wowote. Hii itapunguza uhasama baina ya matabaka. Tabaka la chini litahisi kuwa linatumikiwa ipasavyo na hivyo usawa katika utoaji wa huduma za serikali utachangia katika kuleta uhusiano chanya baina ya matabaka.

**Mwajiriwa kama mwenye Kisasi**

Kisasi ni nia ama kusudio la kulipiza ubaya aliofanyiwa mtu. Ni malipo kwa ajili ya tendo baya alilofanyiwa mtu (*Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, 2004). Kulipiza kisasi mara nyingi huonekana kama njia

ambayo inatuongoza kwenye hali ya utulivu (Ramirez, 2021). Mtu akikukosea au kukuumiza, ni jambo la kawaida kukasirika na kutaka aadhibiwe kwa sababu ya alichofanya. Kuna wakati ambao watu hulipiza kisasi kwa kufanya tendo lile lile walilotendewa na wakati mwingine, tendo la kisasi hukita mizizi. Katika mazingira ya kazi wafanyakazi husikika wakiapa namna watakavyotoroka na bidhaa za waajiri wao wanapokosewa hasa malipo yanapochelewa ama wanaponyimwa malipo yao.

Marx anadai kuwa, ubepari utajiharibu wenyewe kwa kujiundia 'silaha' itakayoumaliza ambayo ni tabaka la wafanyakazi. Tabaka hili haliishi kung'ang'ana kujikomboa kutoka kwa umaskini. Mfanyakazi anapohisi kuwa amedhulumiwa kazini na kunyimwa haki, hutafuta njia yoyote ya kulipiza kisasi (Ball na Dagger, 2005). Matendo ya ulipizaji kisasi yanadhihirika katika riwaya za *Kuli* na *Pendo La Karaha*.

Kwa kawaida, mwajiri ni mtu anayeheshimiwa na waajiri wake. Wao hunyenyekea mbele yake hata anapokuwa mgomvi ama mpyaro kwa kuhofia kupoteza kazi zao wanapokuwa wagomvi na wapyaro machoni mwake. Tunaamini kuwa, mfanyakazi anapoamua kutonyenyekea na kulipiza kisasi kwa kumtusi ama kumpiga mwajiri wake, huwa amefika kilele cha hasira kutokana na maudhi anayofanyiwa na kuona suluhu inayobaki ni kisasi tu bila kujali mustakabali wake. Katika riwaya ya *Kuli,* tunaelezwa kuwa

> Mfano 9:
> Mshihiri yule alikuwa mkali, jeuri na safihi. Alitukana matusi mabaya mabaya akiwa anafanya masihara ya kweli humo humo. Wachukuzi walio majabari walimjibu na yeye akazidi kuwatukana kila walipomjibu.
>
> (uk.13)

Katika dondoo hili, tabia ya wachukuzi kumjibu Mshihiri ambaye ni mkubwa wao kazini inadhihirisha kuwa ni wenye kisasi kwa mkubwa wao.

Tunaendelea kuona, Rashidi anapoanza kazi ya ukuli, anastaajabu siku moja wanapokuwa wakipakia mizigo yenye bidhaa zinazofaa kuenda nchi nyingine, anaona kuli mmoja akivunja sanduku na vitu kutawanyika, wanakula samaki wote waliomo na kuendelea kubomoa masanduku mengine na kunywa bia. Wanavunja masanduku yenye nguo pia na kila mtu anachukua anachokipenda (uk.59). Matendo haya ya wafanyakazi, kando na kuwachora kama wenye kisasi, wanatokea kama wasio waaminifu kazini. Ni kweli kuwa, wakubwa wao wangekuwa wakiwalipa mishahara wanayostahiki na vilevile kuwepo kwa mahusiano bora kati yao, kusingekuwa na tukio la wafanyakazi kuwakosea wakubwa wao kwa kuharibu na kuiba bidhaa.

Katika kisa kingine, George anawafumania wafanyakazi wakiwa katika mazungumzo. Mfanyakazi mmoja anamwonya dhidi ya kuwapigia kelele kama watoto naye George anarudisha,

> Mfano 10
> "Funga mdomo yako *you bloody fool!"*
> Nani unaambia *blal ful ng'ombe we!*" yule mfanyakazi alijibu na hapo George na mfanyakazi huyo walivaana maungoni na kuanza kububurushana. Yule mfanyakazi alimzidi nguvu George na haikuchukua muda alimtupa chini.
>
> (uk.150)

Dondoo hili linatuonyesha namna wafanyakazi walivyochoshwa na tabia ya mkubwa wao na mmoja wao kuamua kuwa jasiri na kupambana na George. Tendo hili na lile la wafanyakazi kumtia mwenzao

shime kwa kusema, "Mpige! Muue! Mnyonge!" kunawasawiri kama wenye kisasi. Ni kweli kuwa, George angekuwa mwajiri mwenye utu, kusingetokea vita hivi. Wafanyakazi wangeamua vita vile kwa haraka bali si kushangilia kwa kumtia mwenzao shime.

Katika riwaya ya *Pendo La Karaha,* uhusiano kati ya mwajiri na mwajiriwa unaonekana kuwa hasi kutokana na matukio ya ulipizaji kisasi. Katika mazungumzo kati ya Kudra na Almasi ambaye ni mfanyakazi wa majirani wa Nayrat na Aminii, Almasi anasema kuwa hajapata mshahara wa miezi sita. Almasi anaendelea kusema bila kuonyesha utani kuwa,

> Mfano 11:
> "Lakini mimi nikipata mali yao, nitachota kisha nikimbie," "Kisha Uarabuni utatoka vipi? Kudra aliuliza. Hayo nitajulia mbele. Wallahi! Siwezi mimi kufanya kazi kama mtumwa!"...
>
> (uk.113)

Katika dondoo hili, maneno ya Almasi yanamsawiri kama mwenye kisasi. Kumwibia mwajiri mali yake kwa sababu ya kutolipwa, ni tendo la ulipizaji kisasi.

Kudra, kwa msaada wa Abdulla, ambaye ni mwajiri wa Almasi anakimbia kazi kwa Nayrat. Kukimbia kwake kunatokana na mateso kama vile: kutolipwa mshahara wake, kupigwa, kutusiwa, kupewa makombo kama chakula, kulala stooni miongoni mwa mengineyo. Kukimbia huku ni tendo la kisasi kwa vile tunaamini kuwa, angekuwa na uhusiano bora na mwajiri wake, angemwarifu kuwa angependa kuondoka na angeondoka kwa amani. Kukimbia kwa Kudra kunaonyesha kuwa amekuwa akikamia sana siku ya kuondokea mateso ya waajiri wake na kuwa hajali nani angemsaidia Nayrat kazi ya nyumba kwa vile anaondoka bila kumwarifu. Isitoshe, anamwiba mwenyeji wake *dirham* zipatazo elfu mia mbili (200,000) kutoka kwa kasha lake. Anaingia kwenye treni huku amevalia buibui na kikapu cha mwajiri wake na miwani ya jua (uk.124).

Tunaamini kuwa mwajiri akiwa na utu kwa mwajiriwa wake, matendo ya kisasi hayatasikika. Tunapendekeza, mwajiri ampe mwajiriwa mshahara unaolingana na kazi anayoifanya bila kuchelewa. Hii ni kwa sababu mwajiri ni mwanadamu pia, mwenye mahitaji ya kawaida kama ya mwanadamu mwingine yeyote. Kando na malipo, ni vyema kumpa mwajiri mazingira bora ya kazi kama vile: malazi mazuri, chakula kizuri na kukosolewa kwa utu anapokosea.

Matendo ya ulipizaji kisasi katika mazingira ya kazi yanadhihirisha uhusiano hasi uliopo baina ya wafanyakazi na waajiri wao. Ulipizaji kisasi unadhihirisha ukweli wa madai ya Marx katika *Communist Manifesto* kuwa, wafanyakazi huungana kupigana na tabaka tawala wanapohisi kuwa wamenyanyaswa vya kutosha. Wao huvamia nyenzo za uzalishaji mali kama vile mashine. Wanaweza wakachoma viwanda wakipigania kurejeshwa kwa mbinu za uzalishaji mali za enzi za kati (Ball na Dagger, 2005).

Marx anapozungumzia Mtazamo wa Historia Kimali, anadai kuwa matendo ya mwanadamu hutegemea hali anayojipata ndani yake katika ulimwengu. Anasema kuwa, viongozi watatawala, wafanyakazi nao watakuwa radhi kufanya kazi hadi kutakapokuwa na mivutano ama uhasama kati yao na waajiri, ndipo wataanza kufanya matendo ya uasi wakipigania mapinduzi (Feur, 1959). Vivyo hivyo, haya yamedhihirika katika riwaya hizi tunapoona matendo ya kulipiza kisasi ya wafanyakazi.

**HITIMISHO**

Makala hii imeonyesha uhusiano uliopo baina ya watu wa tabaka la juu na la chini. Tumegundua kuwa, uhusiano huu ni hasi kutokana na matendo kama vile: unyonyaji, ubinafsi na tabia ya mwajiri ya

kuwa mtesi. Aidha, imebainika kwamba, tabaka la juu linalohusisha waajiri na watawala lina tabia ya kutowajibika katika majukumu yake na hivyo kuchangia katika uhusiano hasi baina ya tabaka la juu na la chini. Kwa upande wa wafanyakazi, mfanyakazi ameonekana kuwa mwenye kisasi anapokosewa kazini kwa kumfanyia mwajiri wake matendo ya kikatili kama vile wizi, vita na hata matusi. Matendo ya kulipiza kisasi yanachangia vilevile katika uhusiano hasi baina ya matabaka haya. Uhusiano chanya kati ya tabaka la juu na la chini haujadhihirika katika uchanganuzi huu. Tumependekeza njia za kuboresha uhusiano kama vile: mwajiri kulipwa stahiki yake baada ya kazi, kukosolewa kwa utu anapokosea na serikali kuwajibika katika majukumu yake ya utawala.

**Marejeleo**

Adam, S. (1979). *Kuli*. Dar es Salaam: Longhorn Publishers.

Ball, T na Dagger, R. (2005). *Ideals and Ideologies*. New York: Pearson Longman.

Barry, P. (2009). *Beginning Theory: An Introduction to Literacy and Cultural Theory (3rd edition)*: Manchester University Press.

Feur, L. (1959). *Marx and Engels: Basic Writings on Politics and Philosophy*. New York: Anchor Books

Habwe, J. (2014). *Pendo la Karaha*. Nairobi: Moran Publishers.

Munyasya, F. (2017). "Mchango wa vijana katika kuleta mabadiliko katika *Kufa Kuzikana na Kidagaa Kimemwozea*." Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa)

Odetola and Ademola (1987). *Sociology: An Introductory African Text*. Hong Kong: Macmillan Publishers.

Ritzer, G. (2008). *Modern Sociological Theory*. New York: University of Maryland.

TUKI.( 2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.

Yunus, M. (2013). "Masuala ya Kisiasa katika Ushairi wa Kandoro: Mifano kutoka Mashairi yake", Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (Haijachapishwa)

**MTANDAO**

https://www. International Labour Organization Conventions between 1919-1960 4th April 2023 2:45 PM

https://www.International Labour Organization. (2019) World Employment Social Outlook: Trends 2019. 3rd April 2023 8:30 AM

https://www. International Labour Organization. (2021) Africa Labour Outlook 2021:Building a Human Centered Future of Work. 3rd April 2023 10:30 AM

https://www.Universal Declaration of Human Rights. (1948) 4th April 2023 12:00 PM

https://www.William Ramirez: Tamaa ya kulipiza kisasi: Septemba 17, 2021